



MZIGO BILA UZITO!

Pr. Marcel KALUNGA MWELA –UBI
Université de Lubumbashi
République Démocratique du Congo

Lugha ni mzigo, lakini ni mzigo wa aina ya pekee. Upekee wake unatokana, hasa, na sababu tatu hizi :

- 1°hauna uzito; na kwa sababu hiyo, haumchoshi anayeuchukua;
- 2°unamsindikiza mtu kila mahali anapoenda;
- 3°kumsindikiza huku kunafanyika bila anayesindikizwa kujua kama ni hivyo.

Kama mizigo mingine, binadamu anaweza kufungua na kutumia vitu vilivyo kuwa ndani mwake kutokana na mahitaji ya mazingira. Kwa mfano, inatakiwa avae mavazi ya pekee wakati wa mvua ambayo ni tofauti na yale ya wakati wa joto ao ule wa baridi kali .

Lakini, pia, kwa sababu tofauti, mtu anaweza akakusudia kulinda mavazi ya wakati wa baridi kunapokuwa joto ao kulinda yale ya wakati wa joto wakati kuna baridi. Hasara ni hasa kwake yeye mwenyewe.

Mambo ni karibu sawa kwa lugha, kwa jumla na , kwa wakati huu, kwa kiswahili. Kwa kuwa sababu ya kwanza ya kuweko lugha ni kumwezesha binadamu kuwasiliana na wengine, basi, inatubidi, kila mara, kukadirisha usemi wetu na kutumia ule unaowezesha kuweko maelewano na yule ao wale tunaotaka kuzungumza nao; kwani kama siyoy, mawasiliano yetu yatakuwa kila mara hatarini .